**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Pili – Tarehe 20 Disemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir:**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuanzishwa kwa Mtandao wa Wabunge wa Afrika wa Kupambana na Rushwa Kanda ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma:**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusiana na Mabadiliko ya Tabia Nchi Zanzibar.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

159. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kipindi cha hivi karibuni matukio ya wizi wa kutumia nguvu, uhalifu wa kutumia silaha za jadi kama visu na mapanga kwa wananchi wasio na makaazi maalumu imeongezeka sana na kuharibu amani na utulivu wa nchi na kuleta hofu kwa jamii.

(a) Kwa kuwa matukio hayo yanaleta picha mbaya kwa Zanzibar Je, ni hatua gani ambazo Serikali imepanga kuzichukua ili kukabiliana na matukio hayo.

(b) Kwa kuwa sheria ya kupiga marufuku kwa watu omba omba ipo ila haitekelezwi na vyombo husika Je, ni jambo gani linalosababisha kutokutekelezwa kwa sheria hiyo.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

46. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika nchi yetu, kuna watu wenye ulemavu wa akili ambao wana mahitaji ya kimwili kama walivyo nayo watu wasio na ulemavu huo. Wengine wamekuwa wakipuuzwa na jamii pale wanapodai kupatiwa wake au waume kwa ajili ya kuoa au kuolewa. Hali hii kwa wasichana wenye ulemavu wa akili, mara nyingi, hupelekea kubebeshwa ujauzito na watu wasiojulikana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatimizia raia kama hawa mahitaji yao ya kimwili na kimaisha.

(b) Je, ikitokezea mmoja katika watu hawa wenye ulemavu au wawili wao wamefunga ndoa, Serikali inawasaidiaje.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

236. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kila mfanyakazi anatakiwa afanyekazi pahala pazuri, penye hewa safi na majengo mazuri. Kwa kuwa Mahkama ya Mkokotoni haikaliki na sio salama kwa wafanyakazi wetu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika Mahkama ile.

(b) Ni lini jengo lile la Mahkama litajengwa.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

121. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kuhakikisha wananchi wanawezeshwa kujitegemea na kujiletea maendeleo yao binafsi, Serikali iliahidi kutoa fedha takriban bilioni 70 kwa wajasiriamali mbali mbali, watu wenye mahitaji maalum na vijana.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kutekeleza ahadi iliyoitoa kwa wahusika hao.

(b) Je, Serikali itasimamia vipi fedha hizo ili kuhakikisha zinatumika kwa makusudio iliyoyapanga.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

27. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali imekuwa ikijitahidi katika kuwahudumia wastaafu wake kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Wizara yenye dhamana ya Fedha. Hata hivyo kumekuwa na ucheleweshwaji wa haki za wastaafu katika ulipaji wa viinua mgongo vyao.

(a) Je, ni kwa nini wastaafu wanacheleweshewa viinua mgongo vyao kutoka Wizara ya Fedha ilhali tarehe zao za kustaafu zinajulikana mapema na si jambo la kukisia wala kubadilika.

(b) Je, huduma ya viinua mgongo, kama ipo, inahusishwa katika programu gani ya bajeti ya Wizara.

(c) Je, ni upi utaratibu unaotarajiwa wa bajeti ya nyongeza (supplementary budget) katika kuwahudumia wastaafu na viinua mgongo vyao.

130. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Miaka mitano sasa tokea Benki ya FBME kusimamishwa kutoa huduma zake hapa nchini ambayo iliruhusiwa kisheria na wananchi wengi walihamasika kuweka fedha zao kupitia taasisi hiyo. Tokea kusimamishwa benki hiyo kumekuwa na ukimya wa muda mrefu sasa na wananchi hawajui nini hatma ya fedha zao.

Je, Serikali inawaeleza nini wananchi ambao wanazihitaji fedha zao ili waweze kujiendeleza kimaisha ikizingatiwa wenzao walioweka fedha zao kupitia MASTER LIFE suala lao limeanza kushughulikiwa na wameanza kupata matumaini ya hatma ya fedha zao.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

55. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuwapatia huduma muhimu wananchi wake kama vitambulisho vya Mzanzibari, vyeti vya kuzaliwa lakini ndani ya Ofisi za Wilaya hasa Kaskazini “A” bado kuna msongamano mkubwa kiasi ambacho wananchi wanavunjika moyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wafanyakazi katika Wilaya ya Kaskazini “A”.

231. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi ya Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kisiwani Pemba kuna eneo liliopo Mava Mabrouk karibu na Sharif Petrol Station ambalo liliandaliwa kwa ajili ya soko la Mnada wa ng'ombe muda mrefu sasa ambapo lilijengwa banda moja lililoezekwa mabati paa moja na kuanza kufanya kazi kwa kipindi kifupi bila ya mafanikio.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kukwamisha ujenzi wa soko lile.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza eneo lile hasa ukizingatia fedha nyingi za walipa kodi zilitumika katika eneo lile.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

7. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa nchi nyingi ulimwenguni zinatumia vituo vya kuendeleza michezo (Sports Academies) ili kuinua vipaji vya michezo mbali mbali katika nchi zao. Na kwa kuwa hata wenzetu Tanzania bara kupitia vituo vya aina hiyo, wametoa wachezaji wazuri wa soka wanaoendelea kusaidia timu zao na Timu za Taifa kama vile Mbwana Samatta, Jonath Mkude, Zimbwe Junior na Shomari Kapombe.

Je, ni lini Serikali itaanzisha vituo vya namna hiyo na hatimae kushajiisha wawekezaji kuwekeza katika tasnia ya soka kwa kujenga vituo vya aina hii.

189. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Uwanja wa Tumbaku uliopo Shehia ya Miembeni umekuwa ukitumika kwa shughuli za michezo hasa mpira wa miguu. Miaka

mingi uwanja ule umekuwa na michanga na vumbi,hali inayozorotesha viwango vya wachezaji wetu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanda nyasi katika uwanja wa Tumbaku.

(b) Je, Serikali kupitia Manispaa ya Mjini ipo tayari kwenda kukagua uwanja wa Tumbaku na kufanya makisio ya gharama za upandaji wa nyasi katika uwanja wa Tumbaku.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

44. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema imeweza kupeleka huduma za umeme hadi vijijini, yakiwemo maeneo ya visiwani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mafundi maeneo ya visiwani hasa ikizingatiwa kuwa umeme unaweza kuleta hitilafu wakati wowote na kuleta madhara makubwa kwa wananchi na mali zao.

238. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika ujenzi wa barabara kuna maeneo mbali mbali yanayotumika kuchimba kifusi kwa ajili ya ujenzi huo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarejesha mashimo hayo katika hali yake ya kawaida ili wananchi waweze kuendelea kuyatumia kama kawaida.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

16. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Katika msimu wa kilimo uliopita wakulima wengi wa mpunga wa mabonde ya Bumbwisudi mazao yao yameharibika kutokana na ubovu wa miundombinu ya umwagiliaji, ukosefu wa pembejeo na uhaba wa mabwana na mabibi shamba. Hali hiyo inaleta shida kubwa ya chakula kwa wakulima wa maeneo hayo.

    (a) Kwa kuwa hali hiyo imesababisha huzuni kubwa kwa wakulima wa maeneo hayo. Je, Serikali inasemaje kuhusu suala hilo.

    (b) Je, Serikali ina mipango gani ya kukabiliana na tatizo kama hilo ili lisitokee tena.

28. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Katika Shehia za Mlindo na Pandani ndani ya Jimbo la Pandani, Serikali imevamia na kuchukua mabonde yakiwemo mashamba ya juu ya wananchi huku ikiwalipa thamani ndogo sana kama fidia za vipando vyao (mfano ni malipo ya TZS 70,000/= kwa kila mnazi). Aidha, katika bonde la Msaani, mashamba ya asili ya wananchi yamekuwa yakikodishwa na wananchi kulazimishwa kuyalipia mashamba yao.

    (a) Je, ni utaratibu upi uliotumika kuwanyang'anya wananchi mashamba yao na kuwalipa thamani ndogo kama fidia.

    (b) Je, Serikali haioni haja ya kutathimini upya mashamba hayo na kuwalipa wananchi ziada ya fidia kulingana na hali halisi ya maisha.

    (c) Je, ni kwa nini JKU wamehodhi eneo kubwa lisilokuwa lao bila kulipa fidia kwa wananchi wenye nyaraka za asili za kumiliki mashamba hayo katika bonde la Msaani.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

23. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mwaka 2014/15 iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano ilikabidhiwa barabara tofauti zilizojengwa na Kampuni mbili tofuati katika Wilaya ya Micheweni. Kampuni ya H-Young ilijenga barabara ya Kinyasini-Wingwi Mapofu-Finya-Mzambarau Takau, Bahanasa-Mtambwe na Kampuni ya MECCO ilijenga barabara ya Wete-Gando na Wete-Konde. Kwa kuwa barabara za Wete-Gando na Wete-Konde zilizojengwa na MECCO zimeanza kuharibika na kufanya mashimo kila sehemu pamoja na kupoteza haiba yake tofauti na barabara zilizojengwa na H-Young ambazo zinaonekana na ubora wa hali ya juu.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea barabara zilizojengwa na MECCO kuharibika mapema mno kulinganisha na barabara zilizojengwa na H-Young Co.

(b) Kwa udhaifu huu wa Kampuuni ya MECCO, Je, Wizara yako inakubaliana na mimi kwamba Kampuni hii ya MECCO haifai kwa sasa kupewa zabuni (tender) za ujenzi wa barabara hasa Kisiwani Pemba.

38. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kuwasaidia wananchi wetu wanaoishi baina ya visiwa vya Unguja na Pemba, Serikali imeendelea kufanya vizuri katika kudhibiti ongezeko la bei ya nauli ya meli na boti za abiria wanaosafiri baina ya Unguja na Pemba. Hata hivyo, kuna malalamiko mengi ya wananchi juu ya tozo za usafirishaji wa mizigo kuwa kubwa na hazijadhibitiwa na Serikali.

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuweka viwango vya tozo ya usafirishaji wa mizigo kwa usafiri wa meli na boti baina ya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

228. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi ya Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kulifanikisha suala la upatikanaji wa elimu kwa watoto wetu, skuli ya Potoa hadi sasa tayari imeshajenga mabanda manne na maktaba moja kwa nguvu za wananchi, ambapo kwa hivi sasa mabanda haya yapo katika hatua ya kuezeka .

Je, ni lini Serikali itakamilisha hatua ya ujenzi iliyobaki katika skuli hii hasa ukizingatia watoto wetu wanapata usumbufu mkubwa katika kufuata elimu katika skuli ziliopo mbali.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

150. MHESHIMIWA ALI ABDULGHULAM HUSSEIN (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Jimbo la Jang'ombe alitoa agizo la kufanyiwa ukarabati kituo cha afya cha Jang'ombe (jumba la vigae) na kuwekwa vifaa vya kisasa ili wananchi waweze kupata matibabu mazuri. Licha ya kutoa agizo hilo na kupokelewa kwa msaada wa vifaa vya ujenzi kutoka NMB pamoja na michango ya viongozi wa Jimbo hilo ambao ni Madiwani, Mwakilishi na Mbunge, mpaka leo hii jengo halijaanza kujengwa.

(a) Wananchi wa jimbo la Jang'ombe wanataka kujua. Je, kuna tatizo gani la kutoanza kwa ujenzi huo.

(b) Serikali inawaahidi nini wananchi hao.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

215. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa maelekezo ya kushushwa bei kwa baadhi ya bidhaa kama nondo, saruji na mchele ambazo zimekuwa zikipanda bei mara kwa mara. Hata hivyo, wafanyabiashara wengi wamekuwa wakipingana na agizo hilo na kupelekea kuuza bidhaa zao kwa bei ya juu ambayo wananchi wanashidwa kuzimudu.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri unasimamia vipi utekelezaji wa agizo hilo.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea wafanyabiashara kushindwa kuuza bidhaa hizo kwa bei elekezi iliyotolewa na Serikali.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

104. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya utalii ndio inayoongoza kuliingizia taifa fedha za kigeni.

(a) Je, ni vyanzo vingapi na ni vipi vipya vya vivutio vya utalii vimeibuliwa kwa miaka ya hivi karibuni

(b) Je, vivutio vingapi vya utalii vimeshaingizwa na kutambuliwa na Gazeti Rasmi la Serikali.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

188. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Eneo la Maisara/Kizingo limekuwa na harakati nyingi za uvuvi na minada ya samaki siku za hivi karibuni. Wavuvi na wanachi wengi hufurika nyakati za asubuhi na mchana kwa shughuli za uvuvi na

kujipatia kitoweo. Hata hivyo, eneo hilo limekuwa halina huduma ya ulinzi kwa nyakati hizo.

(a) Je, Serikali imefikiria kuliwekea ulinzi eneo hilo kwa kuwa shughuli za kiuchumi zinafanyika kwa wingi.

(b) Kwa kutokuwepo ulinzi katika eneo hilo. Je, Serikali haioni kuwa wahalifu wanaweza kutumia mwanya huo kufanya vitendo vya kiuhalifu.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

123. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuna mitaro inayofura maji machafu yenye kinyesi inayoleta kero kwa wakaazi na wapita njia katika maeneo ya Mchina, ambayo pia ni hatari kwa afya na kuleta maradhi ya mripuko hususan katika kipindi cha mvua.

Je, ni sababu zipi zinazolizuia Shirika la Nyumba kuifanyia marekebisho mitaro hiyo.

## III. HOJA ZA MJUMBE:

**Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir:**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuanzishwa kwa Mtandao wa Wabunge wa Afrika wa Kupambana na Rushwa Kanda ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma:**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusiana na Mabadiliko ya Tabia Nchi Zanzibar.

**Zanzibar,**
**20 Disemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**